**OFISI YA RAIS TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA CHALINZE**
**SHULE YA SEKONDARI LUGOBA**

Shule ya Sekondari Lugoba,
S.L.P. 81,
**CHALINZE.**

**Kumb: NA.LSS/F.V 2022/2023** Tarehe 06/04/2022

MWANAFUNZI---------------------------------------------------------------.

SHULE YA SEKONDARI -------------------------------------------------

NDUGU,

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023**

1. Napenda kukuataarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022/2023. Tahasusi ya ...................... Shule ya Sekondari Lugoba ipo Mkoa wa Pwani katika Halmashauri ya Chalinze. Ipo umbali wa kilometa kama 20 kutoka mji wa Chalinze barabara kuu kuelekea Arusha/Tanga.

2. Muhula wa masomo unaanza tarehe........................ Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ....................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe .....................

3. Kwa wanafunzi wenye matatizo ya kiafya walete cheti cha kupimwa Afya kutoka hospitali ya serikali.

4. Kabla hujaanza safari ya kuja shuleni soma maelekezo yote vizuri, kama unadhani hutaweza kutekeleza au kuishi kwa kufuata maelekezo na taratibu hizo, ni vema mzazi akatafuta shule itakayokubaliana na utakavyo.

Mkuu wa Shule na wafanyakazi wote wa Shule hii wanakupongeza na wanakutarajia uwe mwanafunzi MTIIFU, NADHIFU, MWAMINIFU na Mshiriki wa kazi zote za nje na ndani ya darasa.

Kwa mawasiliano waweza piga namba **0787378081 au 0754898202**

**KARIBU SHULE YA SEKONDARI LUGOBA**

**……………………………………….**
**ABDALLAH A SAKASA**
**MKUU WA SHULE**

5. **<u>SARE ZA SHULE</u>**

**WASICHANA**

(a) Sketi za kijani ndefu zinazopita magoti 2 mshono wa Rinda ya V mbele.
(b) Shati nyeupe mikono mirefu 2.
(c) Sketi "Dark blue" za kutosha kwani ndiyo mavazi pekee yanayotumika shuleni nje ya darasa. Mshono wa Rinda ya V mbele
(d) Fulana (TShirt) nyeupe shingo duara za kutosha za kuvaa wakati wote nje ya darasa, zisiwe na maandishi yoyote.
(e) Viatu vyeusi vyenye gidamu (visigino vifupi) na soksi nyeupe.
(f) Aje na doti mbili za kanga au vitenge.
(g) Aje na Shuka 02 rangi ya kijani na Chandarua, vitanda vyetu ni futi 3 x futi 6)
(h) Waislam wanaruhusiwa kuvaa hijab nayo ni Sketi ndefu, nusu kanzu na kijuba cha rangi nyeupe kinachofunika kifua, urefu wa kijuba ni mwisho wa mikono ikinyooshwa kwenda chini.
(i) Nguo za Michezo – Bukta, suruali ya michezo na Fulana: Wanafunzi Mchepuo wa PCM waje na Rangi ya Bluu, PCB rangi Nyekundu, CBG rangi ya Kijani na HGL rangi ya Njano.
(j) Aje na godoro lenye vipimo vifuatavyo unene inch 4,upana futi 3 na urefu futi 6

6. **WAVULANA:**

(i) Suruali nyeusi zenye marinda mawili mbele kila upande.
(ii) Mkanda mweusi
(iii) Shati jeupe mikono mirefu 2.
(iv) Suruali "dark blue" za kutosha kwani ndiyo mavazi pekee yanayotumika shuleni nje ya darasa, marinda mawili mbele kila upande.
(v) Fulana (T Shirt) nyeupe shingo duara za kutosha za kuvaa wakati wote nje ya darasa, zisiwe na maandishi yoyote.
(vi) Viatu vyeusi vyenye gidamu na soksi nyeusi.
(vii) Aje na Shuka 02 rangi ya bluu na Chandarua, vitanda vyetu ni futi 3 x futi 6)
(viii) Nguo za Michezo – Bukta, suruali ya michezo na Fulana: Wanafunzi Mchepuo wa PCM waje na Rangi ya Bluu, PCB rangi Nyekundu, CBG rangi ya Kijani na HGL rangi ya Njano
(ix) Aje na godoro lenye vipimo vifuatavyo unene inch 4,upana futi 3 na urefu futi 6

NB: 1. ***NGUO ZA NYUMBANI, SIMU NA NGUO ZA KUBANA HAVIRUHUSIWI KABISA KATIKA SHULE HII.***

2. ***UREFU WA SURUALI NI HADI IFUNIKE SOKSI, SURUALI FUPI HAZIRUHUSIWI KABISA.***

**ADA NA MICHANGO INAYOTAKIWA KULIPWA NA MZAZI**

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI | MALIPO KWA MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | ADA YA SHULE | 70,000.00 | KWA MWAKA |
| 2. | UKARABATI NA SAMANI | 15,000.00 | KWA MWAKA |
| 3. | KITAMBULISHO NA PICHA | 6,000.00 | HULIPA MARA MOJA |
| 4. | TAALUMA | 20,000.00 | KWA MWAKA |
| 5. | KULIPA WATUMISHI WASIO NA AJIRA YA SERIKALI- VIBARUA | 30,000.00 | KWA MWAKA |
| 6. | DAWA ZA ZAHANATI YA SHULE | 10,000.00 | KWA MWAKA |
| 7. | MITIHANI YA NDANI NA MAJARIBIO | 20,000.00 | KWA MWAKA |
| 8. | TAHADHARI (HAITAREJESHWA) | 5,000.00 | HULIPWA MARA MOJA |
| | **JUMLA KUU** | **176,000** | |

Lipia Benki yoyote ya NMB akaunti namba 21101200009 LUGOBA SECONDARY SCHOOL FUND. Na kisha wasilisha nakala halisi ya benki (Bank Pay in Slip). Mwanafunzi atapokelewa endapo tu amelipa fedha hizo zote au angalau shilingi **141,000/= kwa kuanzia.**

- Kwa wanafunzi wanosomeshwa na Serikali waje na uthibitisho toka kwa Mkurungenzi wa Wilaya anayotoka.
- Wafadhili wengine wakulipie kabisa.

## MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI NI:

1. Ream ya karatasi za photocopy 2 (kwa mwaka)
2. Kila mwanafunzi aje na vitabu vya kujisomea kulingana na mchepuo wake. Shuleni vipo vichache.
3. Vifaa vya masomo ya sayansi kama "Scientific Calculators" n.k.
4. Kwa watakaosoma biolojia waje na "Dissection Set".
5. Kwa watakaosoma kemia na fizikia waje na "stop watch"

6. Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe) visiwe vya plastic.
7. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
8. Vifaa kwaajili ya usafi - Mchepuo wa PCM waje na ***SQUIZER,*** PCB waje na ***HARD BROOM***, CBG waje na ***HARD BROOM*** na HGL waje na ***SOFT BROOM***.

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kupiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na vywele fupi wakati wa wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
(vii) Kufuga ndevu.
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumzi ya madawa ya kulevya.
(ix) Uvutaji wa sigara.
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xv) Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa.
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kuywa sumu n.k.
(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUINGIA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI LUGOBA**

**SEHEMU A (Ijazwe na Mwanafunzi).**

Mimi (Jina Kamili ) ---------------------------------------------------------
Nilizaliwa tarehe ----------------- mwezi ------------ mwaka -----------------------
Dini ---------------------------------Katika Kijiji cha -------------------- ---------wilaya ------------------------------------------

Nakubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha TANO Shule ya Sekondari Lugoba. Nathibitisha kuwa nitatii na kuzifuata sheria zote za Shule ambazo mwanafunzi analazimika kutekeleza na kutimiza ikiwa ni pamoja na **kutokuwa na simu wala kuvaa nguo za nyumbani wakati wote nikiwa shuleni**. Najua na kuamini kuwa migomo na vurugu si njia sahihi ya kutatua matatizo katika jamii hivyo naahidi kutoshiriki katika migomo wala vurugu zozote bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa uongozi wa Shule ili uweze kutatua au kutafutia utatuzi wa changamoto zozote zitakazojitokeza Shuleni.

Saini ---------------------------------------------------------

**SEHEMU B:** (**Ijazwe na mzazi)**

Mimi (Jina kamili) -------------------------------------------------------
wa Kijiji cha ------------------------------ wilaya ya ----------------------------
Dini---------------------------------------- Kazi-----------------------------------
Nafurahi kupokea nafasi aliyopata mtoto wangu. Nitatekeleza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya shule. Pia nitahakikisha mtoto anaenda Shule muda uliopangwa na nitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na Shule kumlea mtoto huyu kinidhamu na kimaadili.

Saini ya Mzazi ------------------------------------------------------

Jina la Mtendaji wa Kijiji-----------------------------------------------

Saini ---------------------------------------------------------------------